# 600 suspected Indian illegal fishermen held

By SAULI GILIARD

AT least 600 suspects have been held for illegal fishing, thanks to strengthened monitoring control and surveillance measures under South West Indian Ocean Fisheries Governance and Shared Growth (SWIOFish) Project.

According to a project report released in Dar es Salaam by the Ministry of Livestock and Fisheries at the weekend, the suspects were arrested following four major land and sea operations mounted along the coastline.

Regions involved in the operations, according to the report presented to editors, are Dar es Salaam, Coast, Lindi and Mtwara. At least 73 cases related to illegal possession of explosives, spears and gas cylinders were also reported.

Under the SWIOFish Project, the report adds: "At least 28 fisheries staff were trained in investigation and field operations on bomb fishing…supported awareness-raising workshops for 72 judiciaries and prosecutors on the impact of blast fishing were conducted."

Other achievements registered under SWIOFish, which is jointly implemented by Tanzania, Comoro and Mozambique, are re-establishment of 50 Beach Management Unit (BMU) groups in five pilot districts namely - Tanga Urban, Pangani, Bagamoyo, Mkinga and Lindi Rural.

Permanent Secretary in the Ministry of Livestock and Fisheries, Dr Rashid Tamatama, told editors that illegal fishing had been controlled by 100 per cent, adding that the involvement of people under BMU groups contributed to such milestone achievements.

"Before SWIOFish Project, only 25 per cent of fishing equipment was registered… until June, this year, the figure doubled to 58 per cent. This is an outcome of an awareness programme," Dr Tamatama said.

SWIOFish is a six-year (June 2015- September 2021) project. The World Bank finances the regional programme which is implemented in Tanzania, Comoro and Mozambique.

Specifically in Tanzania, the programme which is jointly implemented by the Ministry of Livestock and Fisheries, Ministry of Agriculture, Natural Resources, Livestock and Fisheries (Zanzibar) and the Deep Sea Fishing Authority (DSFA) focuses on six priority fish species.

The programme report names priority fisheries as tuna and tuna-like species, prawns, reef fishes, small and medium pelagic species and octopus.

After being sworn in as Minister for Foreign Affairs and East African Cooperation recently, Prof Palamagamba Kabudi, underlined his ministry's priorities of which the blue economy was among his strategic areas.

He said the Ministry would ensure the country's economy brought about desired socioeconomic changes, touching on employment generation, uplifting the business environment and guaranteed the supply of raw materials for local industries.

To ensure this dream comes true, Prof Kabudi said the government would work with various stakeholders, including Indian Ocean Rim Association (IORA), Indian Ocean Tuna Commission (IOTC) and Southwest Indian Ocean Fisheries Commission (SWIOFC).





Scanned with CamScanner

Nipashe, Tarehe 24/11/2020 Uk. 9



Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Elisante Ole Gabriel (mwenye miwani), akizindua kampeni za upandikizaji wa mimba kwenye ng'ombe wa kienyeji katika Kata ya Bugwema Wilaya ya Musoma mkoani Mara juzi, kwa lengo la kuongeza ubora na wingi wa mifugo. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Wafugaji watakiwa ushirikiano kufanikisha mkakati ufugaji kisasa

**Na Sabato Kasika**

WAFUGAJI wametakiwa kutoa ushirikiano kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, ili kufanikisha mkakati wa miradi ya ufugaji wa kisasa wa ng'ombe bora wa maziwa na nyama laini na ngozi nzuri kwa ajili ya soko la uhakika.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Mifugo), Prof. Elisante Ole Gabliel, ndiye aliyasema hayo mwishoni mwa wiki, wakati akizindua kampeni ya uhimilishaji wa ng'ombe katika Wilaya ya Musoma mkoani Mara.

Uhimilishaji huo ulifanyika Kata ya Bugwema na kuhudhuriwa na viongozi wa wilaya hiyo, wafugaji, wawakilishi kutoka ofisi ya mbunge wa Musoma Vijijini na wadau wengine wa sekta ya mifugo.

Prof. Ole Gabriel alisema, lengo la uhimilishaji huo ni upandikizaji kwa kuweka mimba kwenye ng'ombe wa kienyeji kwa kuweka mbegu za ng'ombe wa kisasa kwa njia ya mrija ili kuongeza ubora na wingi wa mifugo.

"Wafugaji toeni ushirikiano kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi ili kuanzisha miradi ya ufugaji wa kisasa wa ng'ombe bora wa maziwa na nyama laini na ngozi nzuri kwa ajili ya soko la uhakika," Prof. Ole Gabriel alisema.

Alisema ni muhimu wafugaji kuzingatia maelekezo yanayotolewa na serikali ili kuachana na ufugaji wa mazoea, badala yake watoe ushirikiano ili kufanikisha mpango huo wa uhimilishaji.

"Kuwa na ng'ombe ni utajiri, hivyo wafugaji wanatakiwa kuwa tayari kuzingatia maelekezo ya serikali, kwa kuwa ina lengo la kuwasaidia kunufaika na utajiri wa mifugo walionayo," alisema.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dk. Vincent Anney, alisema, ofisi yake kwa kushirikiana na idara ya mifugo, watafanyia kazi kilichosemwa na katibu huyo, kwa kuhimiza wafugaji kufuata maelekezo ya serikali.

"Kwa niaba ya wakazi Wilaya ya Musoma wakiwamo wafugaji, tunakushuru na tunaahidi kufuata maelekezo uliyoyatoa kwa wafugaji kwa kuwahimiza waendelee kuyazingatia ili wanufaike," alisema Dk. Anney.

Alisema, Kata ya Bugwema ni miongoni mwa kata 21 za wilaya hiyo yenye wafugaji wengi wa ng'ombe na kwamba ndiyo maana uhimilishaji umefanyika eneo hilo.

Scanned with CamScanner

# Mpango wa kufuatilia kero wavuvi wadogo 'wapikwa'

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

SERIKALI imeandaa mpango wa kitaifa wa kutekeleza mwongozo wa hiari wa kuhakikisha uvuvi mdogo unakuwa endelevu na kutatua kero zinazowakabili wavuvi nchini.

Akizungumza katika kikao kazi cha kupitia mpango huo wa kitaifa jijini hapa, Kaimu Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Uvuvi, Emmanuel Bulayi, alisema bado wananchi wengi wanaojishughulisha na shughuli za uvuvi ni maskini.

Alisema hali hiyo haikubaliki na ni kinyume na maelekezo ya sera na miongozo mbalimbali ya maendeleo ya kitaifa ya nchi ikiwamo Sera ya Uvuvi ya Mwaka 2015.

"Tumeona ni vyema wadau wa sekta ya uvuvi kutoka maeneo mbalimbali kukutana kujadili na kupitisha rasimu ya mpango wa kitaifa wa kutekeleza mwongozo wa hiari wa kuhakikisha uvuvi mdogo unakuwa endelevu nchini," alisema.

Alibainisha kuwa sekta ya uvuvi inatoa ajira ya moja kwa moja kwa wavuvi wadogo wapatao 202,053 na zaidi ya wananchi milioni 4.5 wanategemea shughuli zinazohusiana na uvuvi ikiwamo uchakataji na biashara ya samaki na mazao mengine.

Bulayi alisema serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kutatua kero zinazowakabili wavuvi ikiwamo uandaaji wa mpango huo. Alisema mwongozo huo umeibua na kutoa njia ambazo zikitumika kikamilifu hali ya kiuchumi na kijamii ya wavuvi wadogo itaboresha kwa kiasi kikubwa, huku rasilimali za uvuvi zikiendelea kuvunwa kwa njia endelevu.

"Usimamizi thabiti wa mwongozo huu unaweza kupelekea kuongezeka kwa ajira, kipato, chakula na lishe na hivyo wavuvi wengi kujikwamua katika umaskini uliopitiliza," alisema Bulayi.

Alishukuru Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) kwa kuandaa na kusimamia utekelezaji wa mwongozo wa hiari na kuhakikisha uvuvi mdogo unakuwa endelevu katika muktadha wa chakula na kuondoa umaskini.

Aidha, alisema pamoja na mwongozo huo kuwa umepangiliwa vizuri, kama utekelezaji wake hautasimamiwa ipasavyo, hautaweza kutoa tija inayotarajiwa. Naye Mwakilishi wa FAO, Dk. Oliver Mkumbo, alisema umuhimu wa mpango kazi kwa nchi ya Tanzania uko wazi ukizingatia sekta ya uvuvi inategemewa na watu wengi kwa shughuli mbalimbali za kujipatia kipato na lishe.

"Tunatambua juhudi za serikali, Tanzania ni miongoni mwa nchi chache zinazotekeleza mpango huu, tunaipongeza serikali na wadau kwa kuona umuhimu wa mpango huu na ni matumaini yangu utasaidia kuleta maendeleo kwa wavuvi na jamii kwa ujumla," alisema Mkumbo.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Shirika lisilo la kiserikali la kusimamia mazingira nchini (EMEDO), Elitrudith Lukanga, aliipongeza serikali kwa kuona umuhimu wa kuwa na mpango huo na kutoa wito kwa mashirika mengine kuhakikisha wanashiriki vyema katika mchakato wa utekelezaji wa mpango huo.

Scanned with CamScanner

Habari 24/11/2020

# Umuhimu wa takwimu sekta za kilimo, ufugaji na uvuvi

Na John Mapepele

SERIKALI ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imeendelea kuandaa mipango mbalimbali ya muda mfupi na mrefu inayolenga kuimarisha uchumi na kupunguza umaskini.

Utekelezaji wa mipango hiyo, umeongeza mahitaji ya takwimu bora kwa ajili ya kufuatilia, kutathmini na kupima mafanikio yanayopatikana.

Kati ya mambo muhimu yaliyopangwa kufanyika katika programu za kuimarisha uchumi na kupunguza umaskini, ni pamoja na kufanyika kwa sensa ya kilimo, mifugo na uvuvi ili kupima mafanikio na maendeleo katika sekta ya kilimo ili kuendelea kuimarisha uchumi wa kipato cha kati unaotegemea viwanda.

Kwa mujibu wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 Sura ya Kwanza, Sehemu "C", Serikali italeta mageuzi ya kilimo, mifugo na uvuvi ili kuwa na uhakika wa chakula na kujitegemea kwa chakula wakati wote sambamba na kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya uchumi.

Katika kipengele cha kwanza, Ilani imesisitiza kuhakikisha uzalishaji unaongezeka katika mazao ya chakula, mifugo na uvuvi kwa ajili ya kujitosheleza kwa chakula na lishe bora.

Kipengele cha pili kinasisitiza kuongeza tija katika kilimo, ufugaji na uvuvi ili kuchochea maendeleo ya uchumi hasa katika sekta za viwanda na huduma.

Katika muktadha huu, Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), inasema takwimu zilizokusanywa katika sensa ya mwaka huu, 2020 zitatumika kupima na kutathmini utekelezaji wa mipango mbalimbali ya kuendeleza sekta ya kilimo mifugo na uvuvi.

Tathmini hiyo ni muhimu kwa kuwa itawezesha kufahamu maeneo ambayo nchi imefanya vizuri na yale ambayo bado yanahitaji kuwekewa juhudi zaidi.

"Takwimu hizo mbali ya kuonesha tulikotoka, tuko wapi, pia zitatuonesha kule tunakotaka kwenda kutimiza malengo ya Taifa ya kuimarisha sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi," anafafanua Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk Albina Chuwa, alipokuwa mkoani Singida hivi karibuni kukagua kazi ya ukusanyaji wa takwimu hizo.

Anasema kwa mara ya kwanza, Sensa hii imefanyika kwa kutumia fursa zinazotokana na maendeleo ya teknolojia hasa ile ya kidigitali, ambayo imeboresha usahihi wa takwimu na kupunguza gharama ya kuzikusanya kwa kwa kiwango kikubwa.

Dk Chuwa anaongeza: "Hivyo kwa kweli tunajivunia kwamba Taasisi yetu ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu iko mstari wa mbele si tu katika kuhakikisha Taifa linakuwa na takwimu sahihi, bali hata katika jitihada za kitaifa za kuhakikisha nchi inaingia na inanufaika na uchumi wa kidigitali".

Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida, Dk Angelina Lutambi anasema sensa ya takwimu ni kitu muhimu kwa kuwa kinawezesha kufanya tathimini kuanzia ngazi ya kaya hadi taifa na kwamba, takwimu sahihi zilizokusanywa kutoka kwenye sekta mbalimbali za kimkakati za mifugo, kilimo na uvuvi nchini zimefanya Tanzania chini ya Uongozi wa Rais John Magufuli kuingia katika kundi la nchi za uchumi wa kati duniani.

Dk Lutambi anasisitiza kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika kijijini Msika katika Kata ya Mgharo mkoani Singida kwamba, madhumuni makuu ya sensa inayofanyika mwaka huu ni kupata taarifa muhimu za kilimo, mifugo na uvuvi zitakazotumika kupanga na kutathmini utekelezaji wa mipango mbalimbali ya maendeleo ya sekta nchini Tanzania.

Anasema ukusanywaji wa takwimu huu ukiwa katika ubora unaostahili, utasaidia kufanya taifa kupaa kwenda uchumi wa juu kabisa katika kipindi kifupi kijacho.

Anafafanua akisema, taarifa za magonjwa ya mifugo na mazao zitaisaidia serikali kuainisha maeneo yanayokabiliwa na visumbufu / magonjwa ili kuchukua hatua stahiki na kupanga mipango ya kudhibiti.

Aidha, taarifa kuhusu uzalishaji wa mazao zitasaidia kujua kiasi cha uzalishaji kwa maeneo husika na kuiwezesha Serikali kupanga upatikanaji wa masoko na uwezekano wa kuanzisha viwanda vya kusindika mazao hayo.

Aidha, Dk Lutambi anasema, taarifa kuhusu upatikanaji na matumizi ya ardhi zitatumika kupanga mipango ya matumizi bora ya ardhi vijijini hivyo zitatumika kutatua migogoro ya wakulima na wafugaji hapa nchini.

Kwa upande wake, Dk Chuwa anatanabaisha kuwa, matokeo ya Sensa ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi yanatarajiwa kuweka msingi imara wa sekta hizi kwa miaka mingi ijayo.

Anasema hii ni kwa kuwa sekta ya kilimo ina umuhimu mkubwa katika mustakabali wa maisha ya binadamu kwa kuwa ndiyo chanzo cha chakula na malighafi zinazohitajika katika viwanda hususani katika awamu hii inayoongozwa na dira ya uchumi wa viwanda.

"Kutokana na umuhimu huo, na kupitia Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia ya Mwaka 2030, sekta ya kilimo ilipewa Lengo la Pili la Kutokomeza Njaa, Kuwa na Uhakika wa Chakula, Lishe Bora na Kukuza Kilimo Endelevu," anasema Dk Chuwa.

Anaongeza: "Aidha, lengo hilo limesisitiza umuhimu wa kuongeza tija katika sekta ya kilimo kwa kuongeza thamani ya mazao na pia, kusisitiza [illegible] bora ya ardhi na ku[illegible] udongo, ili kuweza [illegible] wa binadamu [illegible] na kuhimili [illegible]ko ya tabianchi [illegible]zaka yakiwemo majanga mbalimbali kama mafuriko na ukame pamoja na majanga mengine ikiwemo ndege waharibifu."

Anasema pamoja na faida za jumla ambazo mkulima atakazozipata, sensa hii itamsaidia mtu mmoja mmoja kutatua changamoto mbalimbali katika kilimo, mifugo na uvuvi hasa upatikanaji wa pembejeo, huduma za ugani, upatikanaji wa masoko kwa mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi.

"Ni muhimu tukafahamu kuwa takwimu sahihi za mifugo, mazao na uvuvi zitasaidia uchangiaji wa malighafi za viwanda vyetu hivyo kukuza uchumi wetu ambao tunautaka wa viwanda," amesisitiza Dk Chuwa.

Aliyekuwa Naibu Waziri wa Kilimo Hussein Mohamed Bashe, alisema katika uzinduzi wa mafunzo ya wadadisi wa sensa ya kilimo, mifugo na uvuvi ya Mwaka wa Kilimo 2019/20, iliyofanyika katika jijini Mwanza Julai, 25 mwaka huu kwamba Mwaka huu 2020, Benki ya Dunia (WB) imetangaza Tanzania kuwa katika kundi la nchi zenye uchumi wa kipato cha kati.

Alisema taarifa hizi zimeleta faraja kubwa kwa sekta ya kilimo kwa kuwa ndiyo iliyotoa mchango mkubwa zaidi katika pato la taifa wa asilimia 26.6 mwaka 2019 na pia inatoa ajira kwa takriban asilimia 66 ya watu wenye uwezo wa kufanya kazi.

"Sekta ya kilimo ilichangia asilimia 24.3 ya mapato ya mauzo nje ya nchi mwaka 2019. Fedha hizi kwa kiasi kikubwa zinatumika nchini katika mambo mbalimbali ikiwemo ujenzi wa miundombinu wezeshi ya barabara, reli, maji, usambazaji umeme na kuimarisha miundombinu ya kutolea huduma za jamii kama vile afya na elimu kili kuimarisha maendeleo ya wananchi," anafafanua Bashe.

Anaongeza kuwa, kwa mujibu wa Ripoti ya Tathmini ya Umaskini Tanzania Bara ya Mwaka 2018, sekta hii ikiendelezwa vyema, ndiyo pekee yenye uwezo wa kuleta maendeleo jumuishi nchini, hivyo kuna umuhimu mkubwa wa zoezi la sensa ya mifugo, mazao na uvuvi likafanyika kwa ubora na kwa umakini unaostahili.

Katika uzinduzi wa mafunzo ya wadadisi wa sensa hii, Mwenyekiti wa Bodi ya Usimamizi ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu Dk Amina Msengwa, anasisitiza kuwa takwimu zina mchango mkubwa katika maandalizi na utekelezaji wa sera na mipango, na katika kufanya uamuzi sahihi unaotakiwa kufikiwa kwa kutumia ushahidi stahiki.

Amesema Sensa ya Mwaka wa Kilimo 2019/20, ni ya tano kufanyika nchini tangu nchi ipate uhuru.

Meneja Takwimu Ofisi ya Taifa ya Takwimu katika Mkoa wa Singida, Naing'oya Kipuyo, anaishukuru Serikali ya Mkoa wa Singida kwa kusaidia kufanikisha kazi hiyo iliyofanyika kwa takriban siku 50 na anawapongeza wananchi kwa kutoa ushirikiano wa kutosha.

Kipuyo anasema taarifa zilizokusanywa kupitia sensa hii ni za kipindi cha kuanzia Oktoba 1, 2019 hadi 30 Septemba 30, 2020 na kuongeza kuwa, Mkoa wa Singida umekamilisha kazi hiyo kwa maeneo.

Anafafanua kuwa, kaya 1087 katika maeneo madogo 90 ya kuhesabia yaliyochaguliwa kwa ajili ya kufanyiwa sensa hii, zilifikiwa.

John Mapepele ni Ofisa Habari wa Mkoa wa Singida. Anapatikana kwa 0784441180.



Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida, Dk Angelina Lutambi (aliyesimama) akizungumza katika mkutano wa uelimishaji kuhusu ukusanyaji takwimu za mifugo, kilimo na uvuvi kijijini Msika, Singida.

Scanned with CamScanner

# Uchumi na BIASHARA

11 NEEMA YAJA SOKO MAHINDI YA NJANO

12 DHAMIRA YA WIZARA KUFUFUA KILIMO CHA KAHAWA MARA



Kilimo kinahitaji takwimu na utalaamu ili kuwa na tija kwa mkulima, jamii na taifa kwa jumla.

Uvuvi ni moja ya shughuli kuu za uchumi katika mikoa ya Kanda ya Ziwa. Pichani ni wavuvi wilayani Sengerema katika Mkoa wa Mwanza.

# Umuhimu wa takwimu sekta za kilimo, ufugaji na uvuvi



Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), Profesa Elisante Ole Gabriel akiwa katika mnada wa Nyamatara Wilayani Misungwi Mkoani Mwanza. (Picha na Maktaba)

Uk 13

Scanned with CamScanner

# Serikali yaleta neema sekta ya uvuvi

**Na Mwandishi Wetu**

MRADI wa Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIOFish), umepata mafanikio makubwa ikiwamo kudhibiti uvuvi haramu.

Pia kupitia mradi huo, kumekuwepo na ongezeko la usajili wa vyombo vya uvuvi na kurekebisha baadhi ya kanuni za uvuvi ambazo zimesaidia kuongezeka kwa samaki wanaovuliwa.

Kwa mujibu wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk Rashid Tamatamah, mafanikio mengine ya mradi huo ni kuongezeka kwa mapato yatokanayo na uvuvi hususan kwenye halmashauri ambako mradi unatekelezwa.

Dk Tamatamah aliyasema hayo jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki wakati wa kikao kazi kati ya wataalamu wa sekta ya uvuvi na wahariri wa vyombo vya habari kuhusu mradi huo unaotekelezwa kwa miaka sita kwa ufadhili wa Benki ya Dunia kuanzia Juni, 2015 hadi Septemba mwakani kwa thamani ya Dola za Marekani milioni 36.

Akifafanua, alisema uvuvi haramu wa kutumia baruti/mabomu umedhibitiwa kwa asilimia 100 kutokana na kuimarishwa kwa doria pamoja na kuongezeka kwa uelewa wa jamii ya pwani kuhusu madhara ya uvuvi haramu.

"Aidha, usajili wa vyombo vya uvuvi umeongezeka maradufu hadi kufikia asilimia 58 kutoka asilimia 25 ya awali kabla ya mradi.

"Hii imechangiwa na usimamizi wa utekelezwaji wa sheria na kanuni za uvuvi," alisema.

Mradi huo unaotekelezwa katika maeneo ya pwani ya Tanzania katika wilaya tano za mfano zikiwamo Mkinga, Tanga Jiji, Pangani, Bagamoyo na Lindi, kabla ya kuongezwa Halmashauri ya Chalinze.

Aliyataja mafanikio mengine ni kuongezeka kwa samaki wanaovuliwa kutokana na kurekebishwa kwa baadhi ya kanuni za uvuvi ikiwamo Kanuni ya Uvuvi ya Mwaka 2009 kuhusu kubadilisha ukubwa wa macho ya nyavu za kuvulia kuwa milimita nane badala ya milimita 10 ambako kumeongeza tija kwa wavuvi wa dagaa maeneo ya pwani.

"Vile vile, baadhi ya samaki waliotoweka wameanza kuonekana, kwa mfano samaki aina ya sangoro na wengineo. Haya ni baadhi ya matokeo ya kuimarika kwa usimamizi wa rasilimali za uvuvi nchini," alisema.

Pia mradi umefadhili mafunzo ya uvuvi endelevu ambayo yamesaidia kuongezeka kwa uelewa kwa jamii ya pwani, pamoja na uanzishwaji wa vikundi 50 vya Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi (BMU) katika wilaya za mfano.

Pia umewezesha utunzaji wa mazingira ya pwani ambako ukataji wa misitu ya mikoko umepungua badala yake mikoko imekuwa ikipandwa katika vijiji mbalimbali kwa lengo la kutunza mazingira. "Usafi wa fukwe katika maeneo ya mradi umeboreshwa na uchimbaji wa mchanga katika fukwe hususan Bagamayo umepungua kwa kiasi kikubwa," alieleza.

Kuhusu mapato, alitoa mfano wa mapato ya Halmashauri ya Wilaya ya Pangani ambayo yameongezeka kutoka Sh milioni 56 mwaka 2016/17 hadi kufikia Sh milioni 235 mwaka 2018/19.

Mbali ya hayo, alisema mradi umewezesha kuandaliwa kwa viwango vya dagaa na mwani vilivyopitishwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS), kuboreshwa kwa miundombinu ya taasisi shiriki ikiwamo Maabara ya Utafiti iliyoko Kunduchi jijini Dar es Salaam, kujenga ofisi tano za BMU na kuboreshwa kwa mfumo wa ukusanyaji wa takwimu za uvuvi ambazo sasa zinakusanywa kwa njia ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Kwa mujibu wa Dk Tamatamah, Mradi wa SWIOFish unatekelezwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Tanzania Bara na iliyokuwa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi Zanzibar, pamoja na Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu. Wanufaika ni wavuvi wa pwani ya Bahari ya Hindi, wakulima wa mwani, wafugaji wa viumbe maji na wachakataji wa mazao ya uvuvi wakiwamo wanawake na jamii ianyozunguka maeneo hayo.

Lengo la mradi ni kuimarisha usimamizi madhubuti wa uvuvi katika ngazi ya kijamii, kitaifa na kimataifa; kujenga uwezo wa nchi kusimamia rasilimali za uvuvi; kuimarisha ushirikiano wa kikanda katika ulinzi wa rasilimali za uvuvi wa Bahari Kuu; kuinua uchumi wa jamii ya watu wa pwani na kuinua Pato ya Taifa kutokana na rasilimali za uvuvi.

Scanned with CamScanner

# Takwimu sahihi za kilimo, mifugo, uvuvi kutumiwa kuwezesha uhakika wa chakula, ukuaji uchumi

SERIKALI ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania [illegible]

[illegible]

Kwa mujibu wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 Sura ya [illegible]

[illegible]

"Takwimu hizo [illegible]" [illegible] Dkt Albina Chuwa, Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, [illegible] mkoani Singida [illegible]



Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dkt Albina Chuwa (aliyesimama), akifafanua jambo katika mkutano wa [illegible] ukusanywaji takwimu za mifugo, kilimo na uvuvi uliofanyika Kijiji cha [illegible], Kata ya [illegible] mkoani Singida.

Dkt Albina [illegible]

[illegible] Dkt Angelina [illegible]

INAENDELEA UK. 14

Scanned with CamScanner